



Tangazo! Sharti ya Chanjo la Mafua Ili Kuhudhuria Shule

Kuanzia mwanzo wa mwaka wa shule wa 2020-2021, chanjo la mafua **itahitajika kwa wanafunzi wote**. Katika janga la COVID-19, chanjo la mafua itakuwa muhimu zaidi ili kupunguza athari kamili ya magonjwa ya sehemu ya kupumua kwa watu, itawalinda watu walio hatarini kutoka ugonjwa mkali, na itapunguza kulemewa kwa mfumo wa kiyafya.

Je ni wanafunzi gani watahitaji kupokea chanjo la mafua?

Wanafunzi kutoka Chekechea ya Awali hadi wanafunzi wa darasa la 12 watahitajika kupokea chanjo la mafua katika msimu huu wa mafua ili kuhudhuria shule.

Wanafunzi wanafaa kupokea chanjo la mafua lini?

Ni lazima wanafunzi wapokee chanjo la mafua kwa msimu wa sasa kabla ya Desemba 31, 2020.

Je wanafunzi wasio na ushahidi wa barua ya kupokea chanjo la mafua watakatanzwa kuhudhuria shule tarehe Januari 1?

Wanafunzi ambao hawajapokea chanjo la mafua kufikia Januari 1, 2021 hawatahudhuria shule.

Je vipi wanafunzi watakojiandikisha shule baada ya Desemba 31?

Wanafunzi wanaojiandikisha upya kati ya Januari 1 na Machi 31 ni lazima wawe na ushahidi wa kupokea chanjo la mafua kwa msimu wa sasa wa mafua (pamoja na chanjo zote zingine zinazohitajika) wanapoanza shule.

Je chanjo la mafua litahitajika kila mwaka au ni kwa mwaka wa shule wa 2020-2021 pekee? Chanjo la mafua sasa ni chanjo linalohitajika ili kuhudhuria shule na litahitajika kuanzia Desemba 31 kwa wanafunzi wote kutoka Chekechea ya Awali hadi darasa la 12 kila mwaka shule.

Iwapo shule yangu itakuwa inatoa mafunzo ya mbali, je wanafunzi bado watahitajika kutimiza mahitaji ya chanjo? Mahitaji ya chanjo ya shule, ikiwamo hitaji la chanjo la mafua ya kimsimu, zitatumika kwa wanafunzi wote wa Massachusetts walioandikishwa katika madarasa ya Chekechea ya Awali hadi madarasa ya 12, bila kujali iwapo wilaya inatoa mafunzo ya kuhudhuria kibinafsi, au inatumia mafunzo ya kuchanganya kuhudhuria na mbali au mfumo wa mbali.